

SALAMU ZA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO  
NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA JUBILEI  
YA MIAKA 25 YA NADHIRI ZA KITAWA ZA BABA ABATE  
PAMBO M. MKORWE (OSB) ABASIA YA ROHO MTAKATIFU  
MVIMWA TAREHE 29 JUNI, 2023

- *Beatus Urassa, Mhasham Baba Askofu Jimbo la Sumbawanga,*
- *Mababa Askofu wote mliopo hapa*
- *Pambo M. Mkorwe Baba Abate wa Abasia ya Mvimwa,*
- *Maabate wote mliopo hapa,,*
- *Ndugu Gerald M. Kusaya, Katibu Tawala Mkoa wa Rukwa,*
- *Kamati ya Usalama Mkoa,*
- *Mhe. Peter Ambose Lijualikali, Mkuu wa Wilaya ya Nkasi,*
- *Kamati ya Usalama Wilaya,*
- *Mapadri wote,*
- *Watawa wa kike na wa kiume,*
- *Viongozi mbalimbali wa Serikali,*
- *Wageni waalikwa,*
- *Waandishi wa Habari,*
- *Mabibi na Mabwana.*

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....

Awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na Baraka kwa kutuwezesha sisi sote kukutana mahali hapa tukiwa wazima na wenye afya njema. Nitumie fursa hii pia kumshukuru sana baba Abate pambo Mkorwe wa Abasia hii ya Mwimwa kwa kunialika kuhudhuria Jubilei yake ya miaka 25 ya nadhiri za Kitawa. Namshukuru sana.

Sambamba na hilo, nimpongeze sana Baba Abate kwa kutimiza miaka 25 ya nadhiri za Kitawa. Miaka 25 ni mingi sana na tunaamini kuwa umefanya mambo mengi sana katika maendeleo ya Kanisa, Wilaya, Mkoa na Nchi kwa ujumla kutokana na maono yako mengi ambayo umeitiwa na Mwenyezi Mungu

**Ndugu Washiriki**, katika kitabu cha Nabii Isaya (6:1-2, 3-8) kinazungumzia wito wa Nabii Isaya mwenyewe namna alivyopokea wito wake wa kuwa Nabii. Isaya anauelezea wito wake katika kipindi maalum cha muda – Mwaka aliokufa Mfalme Uzia. Kwa hili anapenda kutuambia wito wake ni kitu halisi kilichotokea, sio habari ya kutunga. Nimwambie tu Baba Abate kuwa wito wake wa kumtumikia Mungu ni kitu halisi na sio cha kutunga ndio maana leo umetimiza miaka 25 ya nadhiri za Kitawa.

**Ndugu Washiriki**, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imekuwa na ushirikiano mkubwa sana na Viongozi wa Dini. Na sisi wasaidizi wake tutakuwa karibu nanyi Viongozi wa Dini ili tuweze kuwatumikia wananchi. Tunatambua

kuwa Abasia hii ya Mvimwa ina mchango mkubwa sana katika eneo hili kwani wamesaidia ujenzi wa shule ya msingi Ntemba na kusaidia jamii masuala mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mazingira. Natambua kuwa ipo Shule ya Msingi Mvimwa ambayo imekuwa ikifanya vizuri sana kwenye Mkoa wetu inayomilikiwa na Abasia ya Mvimwa, haya yote yanafanyika chini ya uongozi wako Baba Abate. Tunashukuru sana.

**Ndugu Washiriki**, Nchi yetu imeendelea kuwa na Amani na Utulivu kama ilivyoasisiwa na Waasisi wetu na ndio maana tumekuwa tukikusanyika kuabudu bila wasiwasi wowote. Niwaombe sana Viongozi wote wa Dini kuendelea kuliombea Taifa letu ili liendelee kuwa na Amani na Utulivu.

**Mwisho**, lakini si kwa umuhimu nimshukuru sana Baba Askofu wa Jimbo la Sumbawanga kwa ushirikiano mkubwa ambao amekuwa akitupatia katika kutekeleza majukumu yetu. Natambua kuwa mlituazima majengo yaliyokuwa yanatumika na Chuo cha Ualimu Sumbawanga. Tunashukuru sana.

Mungu Ibariki Tanzania,  
Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa,  
Mungu Bariki Kanisa Katoliki  
Asanteni sana kwa kunisikiliza

Charles Makongoro Nyerere  
**MKUU WA MKOA WA RUKWA**